Tanzania
Hutoa baadhi ya taarifa zinazohusu bajeti kwa umma katika mwaka wa fedha.

Ripoti ya Utafiti wa Uwazi wa Bajeti 2012

HakE Kijarida, 1K, 2013

KATI YA 100	ALAMA ZA KIPIMO CHA UWAZI WA BAJETI
80-100 ya kina	47
61-80 Inayoridhisha	
41-60 Baadhi	
21-40 Kidogo	
0-20 Kidogo mno	

Tuko wapi baada ya mwaka 1 wa Mpango wa Kimataifa wa Kuendesha Shughuli za Serikali kwa Uwazi (OGP)

Ipi nafasi ya Tanzania ukilinganisha na nchi jirani?



Ni zipi kati ya nyaraka 8 muhimu za bajeti ambazo wananchi huzipata?

	Maelezo ya nyaraka	Mwaka 2008	Mwaka 2010	Mwaka 2012
1	Taarifa ya Kabla ya Bajeti (PBS)	Iliandaliwa; lakini haikuchapishwa	Iliandaliwa; hai-kuchapishwa,	Ilichapishwa
2	Mapendekezo ya bajeti ya Serikali (EBP)	Ilichapishwa	Ilichapishwa	Ilichapishwa
3	Bajeti iliyopitishwa (EB)	Ilichapishwa	Iliandakiwa; hai-kuchapishwa	Ilichapishwa
4	Bajeti ya Wananchi (CB)	Haikuandaliwa	Haikuandaliwa	Ilichapishwa
5	Taarifa za ndani ya Mwaka(IYR)	Ilichapishwa	Ilichapishwa	Ilichapishwa
6	Mapitio ya Nusu Mwaka (MYR)	Haikuandaliwa	Haikuandaliwa	Haikuandaliwa
7	Ripoti ya Mwisho wa Mwaka(YER)	Haikuandaliwa	Haikuandaliwa	Haikuandaliwa
8	Taarifa ya Ukaguzi (AR)	Ilichapishwa	Ilichapishwa	Ilichapishwa

Kutoka 0 hadi 100: Je, Tanzania imeongeza kiwango cha taarifa inazozitoa katika ya nyaraka 8 muhimu za bajeti?



Kipimo cha Uwazi wa Bajeti (OBI)

Ripoti ya Uwazi wa Bajeti hupima iwapo serikali kuu, katika kila nchi iliyofanyiwa utafiti, hutoa nyaraka nane muhimu za bajeti kwa umma. Utafiti huu pia hupima iwapo taarifa zilizomo katika nyaraka hizo ni za kina, zimetolewa kwa wakati na zenye manufaa. Utafiti huu hutumia vigezo vinavyokubalika kimataifa kupima uwazi wa bajeti kwa kila nchi. Vigezo hivyo vilianzishwa na mashirika ya kimataifa kama vile Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), Shirika la Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo (OECD), na Shirika la Kimataifa la Ushirika wa Wakaguzi wa Kimataida (INTOSAI).

Tanzania imepata alama 47 kati ya 100, ambazo ni kubwa kiasi kushinda wastani wa alama 43 kwa nchi zote 100 zilizofanyiwa utafiti. Lakini alama ilizopata Tanzania ni ndogo ukilinganisha na alama zilizopata nchi jirani za Kenya na Uganda. Alama ilizopata Tanzania zinaashiria kuwa serikali hutoa baadhi tu ya taarifa za bajeti ya serikali ya kitaifa na shughuli za kifedha katika mwaka wa bajeti. Hali hii inaleta ugumu kwa wananchi kuiwajibisha serikali juu ya usimamizi wa fedha za umma.

Tuko wapi baada ya mwaka mmoja wa utekelezaji wa Mpango wa Kimataifa wa Kuendesha Shughuli za Serikali kwa Uwazi (OGP)?

Mpango wa Kimataifa wa Kuendesha Shughuli za Serikali kwa Uwazi ni mkakati wa kimataifa unaolenga kuboresha uwazi, kuwawezesha wananchi, kupinga rushwa na kuchochea matumizi ya teknolojia mpya katika kuboresha utawala. Tanzania imejiunga na mpango wa OGP Septemba 2011. Ni wakati muafaka kwa serikali kutumia alama za Kipimo cha Uwazi wa Bajeti kujipima kama Tanzania inapiga hatua katika utekelezaji wa malengo yaliyoorodheshwa kwenye mpango wa utekelezaji wa OGP.

Tanzania ifanye nini kuongeza alama?

Alama za Tanzania katika Kipimo cha Uwazi wa Bajeti zinaongezeka katika kila awamu ya utafiti wa uwazi wa bajeti. Hali hii inatia moyo na serikali haina budi kupongezwa kwa hili. Lakini, kupata alama 47 kati ya 100 katika Kipimo cha Uwazi wa Bajeti cha mwaka 2012, serikali ya Tanzania haina budi kuongeza kiwango cha uwazi katika bajeti kwa kuchukua hatua za muda mfupi, ambazo baadhi yake zinaweza kutekelezwa bila gharama yoyote kwa serikali.

Mapendekezo

- Kuweka wazi Taarifa ya Mapitio ya Nusu Mwaka na Ripoti ya Mwisho wa Mwaka. Kwa mujibu wa Utafiti wa Uwazi wa Bajeti wa mwaka 2012, nchi 29 huweka wazi taarifa za mapitio ya nusu mwaka ikiwemo nchi jirani ya Uganda, na nchi 72 huweka wazi ripoti za mwisho wa mwaka, pia ikiwemo Rwanda na Uganda

- Kuongeza uelewekaji wa Mapendekezo ya Bajeti ya Serikali, hasa kwa kuzingati utoaji wa taarifa katika maeneo yafuatayo:
    1. Matumizi katika mchanganuo wa kikazi kwa mwaka uliopo na uliopita na pia makisio ya matumizi kwa miaka ijayo.
    2. Makisio ya mapato kwa miaka miwili baada ya mwaka wa bajeti na mapato yasiyokatwa kodi ya mwaka uliopita.
    3. Taarifa kuhusu kiwango na mchanganuo wa deni la serikali kwa mwaka wa fedha na mwaka uliotangulia.
    4. Utabiri wa kiuchumi na makisio yaliyotumika kuandaa bajeti.
    5. Maelezo ya kisera na vipimo vya kiutendaji.
    6. Fedha zilizo nje ya bajeti, madeni ya kimatumizi, madeni tarajiwa na yajayo, mali ya kifedha na isiyo ya kifedha, matumizi ya kodi na asilimia iliyoelekezwa katika vipengele vya siri.

- Kuongeza uelewekaji wa maelezo ya kabla ya bajeti kwa kuhusisha maelezo ya mjadala na makadirio ya kiidadi ya fedha za serikali na sera za kiuchumi za mwaka wa fedha unaofuata.

- Kuweka wazi Bajeti ya Wananchi katika hatua zote nne za mchakato wa bajeti(uundwaji wa bajeti, kupitishwa kwa bajeti, utekelezaji wa bajeti na ukaguzi wa hesabu za serikali).

- Kuongeza uelewekaji wa bajeti iliyopitishwa na Bunge kwa kuweka maelezo ya kina katika ngazi za programu.

“BAJETI ZILIZO WAZI HUBADILI MAISHA”

IBP | INTERNATIONAL BUDGET PARTNERSHIP
Open Budgets. Transform Lives.

hakielimu